

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA.
HALMASHAURI YA MJI WA TARIME.

12/10/2022.

**TANGAZO LA KAZI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 41 KATIKA
SHULE MPYA ZA SEKONDARI ZA HALMASHAURI YA MJI TARIME.**

MAOMBI YA KAZI YA UJENZI KWA LOCAL FUNDI.

Kwa: WANANCHI WOTE.

Halmashaurya Mji Tarime S.L.P 45 Tarime, imepokea fedha toka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 41 katika shule sekondari kwa kutumia njia ya Force Account.

2. Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji Tarime anawatangazia mafundi wote (local Fundi) wenye uwezo wa kufanya kaziya ujenzi kutuma maombi yao.

3. Unakaribishwa kuleta maombi yako kwa ajili ya kazi ya ujenzi kama ilivyoelezwa kwenye Maelezo ya kazi hapo chini;

S/n	Kazizitakazofanyika
i.	Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa.
Ii	Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa.

4 .SIFA ZA MWOMBAJI;

Mwombajinilazima awe na sifa zifuatazo;-

- i) Awe raiawa Tanzania
- ii) Awe naujuzi wa kazi husika
- iii) Awe amewahi kufanya kazi za ujenzi/ukarabati wa majengo ya serikali
- iv) Awe naAkaunti Bank

5.VIAMBATANISHO;

Waombaji wote ni sharti waambatanishe vitu vifuatavyo;-

- i) Barua ya utambulisho toka kwa mwenyekiti wa mtaa au mtendaji wa mtaa anapoishi.
- ii) Kitambulisho cha mpiga kura au leseni ya udereva.
- iii) Mikataba ya kazi alizowahi kufanya kabla ya tangazo hili au cheti cha malipo (certificates)
- iv) Taarifa ya kibenki (Bank statement) au kadi ya benki yenye majina halisi ya mwombaji.

6. Barua zote za maombi nilazima zipelekwe ofisi ya Mkurugenzi wa mji S.L.P 45 Tarime, zitapokelewa Ofisi ya Ugavi Halmashauri ya mji Tarime.

7. Nyarakaza kazi hizo kwa Lugha ya **Kiswahili** zitatolewa katika ofisi ya ugavi bila malipo yoyote. *Kwa Malipo ya Tsh 20,000/-*

8. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni Siku ya **jumanne** Tarehe **18/10/2022**, kablaya Saa **4.00 Asubuhi**. Maombi yote yatafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi au waombaji walioamua kuhudhuria katika kikao cha ufunguzi **Ofisi ya ugavi**.

9. Maombi yatakayochelewa hayatapokelewa kwa namna yoyote ile.

.....
Gimbana E, Ntavyo.
Mkurugenzi wa Mji,
Tarime.



Soma Moya

ORODHA YA SHULE ZINAZOJENGEWA MADARASA.

NA	JINA LA SHULE	KATA
1.	SHULE YA SEKONDARI BOMANI	BOMANI
2.	SHULE YA SEKONDARI TURWA A”	TURWA
3	SHULE YA SEKONDARI TURWA B”	TURWA
4.	SHULE YA SEKONDARI IGAGANA	SABASABA
6	SHULE YA SEKONDARI NKENDE	NKENDE
7	SHULE YA SEKONDARI NYAMISANGURRA	NYAMISANGURA
8	SHULE YA SEKONDARI TAGOTA	KENYAMANYORI
9	SHULE YA SEKONDARI KENYAMANYORI	KENYAMANYORI
10	SHULE YA SEKONDARI NYANDOTO	NYANDOTO
11	SHULE YA SEKONDARI MOGABIRI	KETARE